**BUKU LA 16**

Salamu kwa Familia ya Wilaya ya Shule za Jimbo la DeKalb,

Ninatumaini kwamba ulikuwa na juma lenye mafanikio. Huku COVID-19 ikiendelea kuathiri maisha ya jamii yetu, ahadi yetu kwa afya na usalama wa wanafunzi na wafanyakazi wetu bado imesalia kuwa muhimu.

Kama nilivyoshiriki wiki chache zilizopita, mpango wetu wa kufungua tena shule hujabadilika na ni thabiti. Njia yetu inayotegemea data ya kufungua tena shule imetuwezesha pia tusifungue tena na kufunga shule, kwa hivyo kufanya jamii yetu isiweze kutabiri zaidi wakati wa janga hili. Ni muhimu nyakati hizi zisizokuwa na uhakika kwamba wanafunzi wetu waendelee kulenga masomo hadi tuweze kurejea masomo ya ana kwa ana kwa usalama. Huku wanafunzi wetu wakiendelea kulenga ufanisi wa elimu, viongozi wetu wa wilaya wanafanya kazi kwa bidii ili kuandaa kufunguliwa tena kwa shule ikiwemo maandalizi ya dharura, usafiri, itifaki za usalama, na zaidi. Tafadhali endelea kutembelea tovuti yetu ya Kufungua tena kwa taarifa https://www.dekalbschoolsga.org/school-reopening/.

**Viwango vya maenezi katika jamii vinaendelea kuongezeka zaidi ya kigezo cha "Maenezi ya Makubwa" ya visa 100 kwa wakazi 100,000 kwa kipindi cha wiki mbili kama ilivyohesabiwa na Idara ya Afya ya Umma ya Georgia (GDPH). Hadi leo, nambari hii iliyoripotiwa na GDPH ya Kaunti ya DeKalb ni 198.** Ili kupata habari mpya kuhusu viwango vya maenezi katika Kaunti ya DeKalb, tafadhali endelea kutembelea: https://dph.georgia.gov/covid-19-daily-status-report. Kuongezeka kwa nambari hizi kunaleta wasiwasi mkubwa na tunataka kuhakikisha kwamba familia na wafanyakazi wetu wamefahamu wazi kuhusu baadhi ya habari muhimu kulingana na Kituo cha Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (CDC).

Fahamu habari kuhusu ugonjwa wa virusi vya korona 2019

- Magonjwa yanaweza kumfanya mtu yeyote kuwa mgonjwa haijalishi umbari au jamii yake.
    - Hofu na wasiwasi kuhusu COVID-19 unaweza kufanya watu kuwaepuka au kuwakataa wengine hata kama hawamo katika hatari ya kueneza virusi.

- Kwa watu wengi, hatari ya moja kwa moja ya kuwa wagonjwa sana kutokana na virusi ambavyo vinasababisha COVID-19 inafikiriwa kuwa iko chini.
  - Baadhi ya watu wanaweza kuwa katika hatari iliyoongezeka ya matatizo zaidi makali yanayotokana na COVID-19 na wanapaswa kuchukua hatua za kujilinda.
  - Mtu ambaye amekamilisha karantini au ameondolewa kwenye mpango wa kujitenga hana hatari ya kuwaambukiza watu wengine.
- Kuna mambo rahisi unaweza kufanya ili kujiweka wewe mwenyewe na wengine salama.
  - Nawa mikono yako kwa sabuni na maji kwa angalau sekunde 20, hasa baada ya kupenga pua lako, kukohoa, au kupiga chafya, kwenda msalani, na kabla ya kula au kuandaa chakula.
  - Epuka kugusa macho, mapua, na mdomo wako kwa mikono isionawishwa.
  - Salia nyumbani ukiwa mgonjwa.
  - Funika mdomo unapokoa au kupiga chafya kwa tishu, kisha uitupe ndani ya pipa.

Tafadhali kumbuka kweli hizi tunapokuwa tukipitia janga hili.

**Siku Katika Maisha**

Tunapokuwa tukiendelea kujiandaa kwa shule kufunguliwa tena, baadhi ya wanachama wetu wakuu wa baraza na wanachama wa bodi walikuwa na nafasi ya kutembelea shule tatu za DCSD ili kufuatilia mpango wa kurudi shuleni wakati wa safari ya “Siku Katika Maisha” wiki hii iliyopita. Safari hii iliwaruhusu wanachama wa baraza kufuatilia uchanganuzi wa itifaki/kanuni za shule, wanafunzi katika mazingira ya darasa, mabadiliko ya wanafunzi, chakula cha mchana na kuruhusiwa kutoka shuleni. Asante kwa wafanyakazi katika Shule ya Msingi ya Canby Lane, Shule ya Kati ya Chapel Hill na Shule ya Upili ya Tucker kwa kuwezesha safari hii.

**Wiki ya Hatua ya 2020 ya Black Lives Matter**

Wiki ya Novemba 9-13 itakuwa ya “Black Lives Matter katika Wiki ya Hatua ya 2020 ya Shule za DeKalb” katika Wilaya. Tukio hili la wiki nzima litakuwa na shughuli za mafunzo shuleni za Black Lives Matter, ikiwemo sherehe za mitandao ya kijamii za Vyuo vya Elimu na Vyuo Vikuu ambavyo Kihistoria ni vya Watu Weusi (HBCUs), adhimisho la biashara zinazomilikiwa na watu weusi katika Kaunti ya DeKalb, Mchuano wa My Brother’s Keeper,

siku ya “My Black is Beautiful Unity Day,” na majadaliano yanayoongozwa na jopo la wanafunzi.

Lengo la “Black Lives Matter katika Wiki ya Hatua ya 2020 ya Shule za DeKalb” ni kuendeleza harakati inayoendelea kuhusu tafakari muhimu na mazungumzo wazi katika jamii za shule kwa watu wa kila umri kushiriki katika masuala ya haki za kirangi.

DCSD ni wilaya ya shule yenye jamii anuwai na tunasheherekea jamii hizo anuwai maridadi kwa njia yoyote ile. Black Lives Matter katika Wiki ya Hatua ya 2020 ya Shule za DeKalb inawapa wanafunzi na wafanyakazi wetu nafasi ya kutambua taswira chanya kwa wanafunzi wetu katika jamii zetu huku tukizungumzia tena dhidi ya udhalimu wa kirangi na kijamii katika jamii zetu.

**Kushiriki kwa Jamii**

Ilikuwa heshima kubwa kwangu kuwa msemaji mgeni wa Rotary Club ya Stone Mountain. Mwaka huu wamekuwa Rotary Club ya kwanza duniani ya Mseto. Mseto ni nini? Rahisi: Wanawapa wanachama wao chaguo la kuhudhuria mkutano ana kwa ana kila wiki au kushiriki katika mtiririko wa moja kwa moja.

Asante kwa kila mtu aliyehudhuria mikutano yetu ya Region Town Halls na Town Hall ya Wazazi wetu jana usiku. Tuna timu nzuri sana inayoongozwa na mikoa na wilaya yetu na ninashukuru kwa jitihada zenu zote. Tutaendelea kuzingatia michango yote na kama ulikosa mkutano wa jana usiku wa town hall, bofya hapa https://youtu.be/0mC36NaRKVQ.

Kuwa na wikendi njema na asante kwa yote unayofanya ili kuhakikisha wilaya yetu ni jamii thabiti.

Shabiki wako wa #1,

Cheryl Watson-Harris